

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE



Kumb. Na.HWK/S.1/24/Vol.III/179

14/07/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe anatangaza nafasi (5) za kazi. Tangazo hili limetokana na barua **Kumb. Na. FA.170/369/01C/12** ya tarehe **23 Mei, 2023** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikihusu idhini ya kutekeleza ikama na bajeti kwa ajira mpya katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Maombi ya kujaza nafasi yoyote kati ya hizo yanakaribishwa kutoka kwa Mtanzania yoyote mwenye sifa zilizotajwa katika Tangazo hili:

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III- NAFASI NNE (4)

MAJUKUMU YA KAZI.

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao; kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na kamati za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji; na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo:- **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS.B kwa mwezi.

2. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - NAFASI MOJA (1)

MAJUKUMU YA KAZI.

- Kupanga na kudhibiti kumbukumbu/nyaraka katika vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Wizara za Serikali na Taasisi zake.
- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka zinazohitajiwa na wasomjaji.
- Kufanyia ukarabati kumbukumbu zilizoharibika.
- Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika vyumba vya kuhifadhia nyaraka

2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Sita (VI) mwenye cheti cha Utunzaji Kumbukumbu katika moja wapo ya fani zifuatazo:- Afya, Masijala, Mahakama na Ardhi kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali .

2.2 MSHAHARA

- Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS.B kwa mwezi.

NB: MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE:

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
3. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, maelezo binafsi, vyeti vya Kidato cha nne au kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa husika na Picha moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma. **Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.**
4. Kwa waombaji waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na/au kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
5. Kwa waliohitimu elimu ya chuo nje ya nchi, wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE).
6. **Testimonials "Provisional Results" Statement of results; hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi; wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
9. Waombaji wote watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili (Interview)
10. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoanishwa hayatashughulikiwa.
11. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **24 Julai 2023 saa 9:30 Alasiri.**
12. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na barua ya maombi isainiwe na kuambatishwa na vielelezo vinavyohitajika na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P. 584,
Korogwe.

Au

District Executive Director,
Korogwe District Council,
P.O. Box 584,
Korogwe.

NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe www.korogwedc.go.tz

Halfan H. Magani
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

